# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

**HALMASHAURI YA WILAYA NACHINGWEA**
**SHULE YA SEKONDARI FARM 17**

***"Elimu ni Ukombozi"***

SHULE YA SEKONDARI FARM 17,
S.L.P 312
**NACHINGWEA**.

***KUMB. NA. F.17SS/……. /……….*** 01/12/2020

MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………………………………….
C/O MWL. MKUU S/M …………………………………………..
S.L.P 49,
**NACHINGWEA**.

**YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI FARM 17 KIDATO CHA KWANZA -2021</u>**

**1.0. UTANGULIZI**

Kwa niaba ya uongozi wa wafanyakazi wote wa sekondari ya Farm 17 nachukua fursa hii kumpongeza mwanao kwa kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari FARM 17. Shule ya sekondari Farm 17 ipo km 4 kutoka barabara ya Kilimarondo baada ya Kijiji cha Kipara km. 30 kutoka Nachingwea. Shule ya sekondari Farm 17 ni shule ya Hosteli ya mchanganyiko, pia inapokea wanafunzi wa kutwa.

- Ndugu mzazi/mlezi kamwe usimnyime HAKI ya kupata ELIMU kijana wako kwa kisingizio cha UMASIKINI au KIPATO DUNI kwani Elimu ni Ukombozi. Aidha kwa kutambua haya serikali ya AWAMU YA TANO inatoa ELIMU kwa kijana wako BURE, Hivyo hauna kisingizio chochote cha kutomleta kijana wako shuleni.
- Shule itafunguliwa JUMATATU ya tarehe **11/01/2021** saa moja kamili na mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/01/2021 baada ya tarehe 20/01/2021kama hutamleta shuleni mtoto wako itakulazimu mzazi/mlezi kuieleza serikali kwa nini isikuchukulie hatua za kisheria kwa kumnyima mtoto wako haki yake ya msingi ya kupata elimu.

Mwisho, pamoja na barua hii naambatanisha viambata A, B, C, D na E. Mzazi/mlezi yakupasa usome, uelewe na kutekeleza ili kutuondolea usumbufu hapo baadae

***"KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI FARM 17"***

……………………..
MKUU WA SHULE

**NAKALA:**

1. Katibu Tawala Mkoa,
   S.L.P 1054
   LINDI

2. Mkurugenzi Mtendaji
   Halmashauri ya (W) Nachingwea
   S.L.P 291,
   NACHINGWEA

*FOMU A*

**1.0. SARE YA SHULE**

- **WAVULANA**
  Suruali mbili za rangi ya khaki na Suruari ya kushindia (damu ya mzee), za kushona zenye mfuko mmoja wa nyuma (isiwe muundo wa jinsi na zinaweza kupatikana shuleni kwa gharama ya sh.19,500/=kila moja). Mashati mawili meupe mikono mifupi, tai ya kaki na viatu jozi mbili vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe jozi mbili. sweta rangi ya kijani mikono mirefu, T-shirt zenye kola za kushindia mbili za rangi ya zambarau (mikono mifupi) zinapatikana shuleni

- **WASICHANA**
  Sketi mbili rangi ya kijani ndefu kupita magoti mshono wa malinda ya kuzunguka, (zinapatikana shuleni kwa gharama ya sh 18,500/=kila moja), mashati mawili meupe mikono mifupi, tai ya kijani, kwa HIJABU ifanane na rangi ya shati na viatu jozi mbili vyeusi vya kutumbukiza vya ngozi vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe. Gauni la damu ya mzee kwa ajili ya kushindia hijabu nayo ifanane na gauni. Aidha rangi na aina ya kitambaa cha sketi kimeambatanishwa katika fomu hii.

  ***NB:***
  (i) T-shirt za kushindia Tsh. 12,000 kwa kila T-shirt zinapatikana shuleni.
  (ii) Viatu vya bajaji haviruhusiwi
  (iii) NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KABISA
  (iv) Mashuka pia yanapatikana shuleni Tsh 18,000/= kwa mawili.

**2.0. SARE YA MICHEZO**

Kwa shule hii sare za michezo kwa wavulana ni bukta na T-shirt nyekundu na kwa wasichana Traksuti za blue au bukta nyekundu pamoja na raba jozi moja kwa jinsia zote

**3.0. VIFAA VYA USAFI**

Hakikisha kijana wako anakuja na vifaa vifuatavyo vya kufanyia usafi
(i) Jembe – Ngwamba mpya na mpini wake
(ii) Fagio
(iii) Ndoo 2 moja lita 20 moja lita 10
(iv) Reki kwa wasichana na panga kwa wavulana
(v) Fyekeo

Vifaa vitakaguliwa pindi mtoto atakaporipoti shule na vikikabidhiwa ni mali ya shule na ni lazima aje navyo siku ya kuripoti shuleni.

**4.0. VIFAA VYA TAALUMA**

- Daftari kubwa kumi (10) counter book) 2Q au 3Q
- Kamusi ya kiingereza (Dictionary)
- Mkebe wenye vifaa vya Hisabati (Mathematical set)
- Kalamu za wino na penseli.
- Rimu moja ya karatasi zisizo na mistari za kufanyia mazoezi na mitihani.

***FOMU B***

**MAHITAJI YA WANAFUNZI WA HOSTELI**

Wanafunzi wa hostel watajigharamia chakula, malazi, matibabu,wapishi na fedha ya mfukoni. Aidha vitu hivi ni lazima anunue mzazi/mlezi au kulipa fedha taslim kwa bei ya sokoni wakati huo.

**MAHITAJI KWA MUHULA 1**

1. Unga wa sembe 50 kg
2. Mchele 5 kg
3. Maharage 30kg
4. Chumvi 2Kg
5. Vitunguu 2000/=
6. Fedha ya mpishi Tsh. 10,000/=
7. Fedha ya matibabu Tsh. 8,000/=
8. Sukari kg 5
9. Mchango wa hosteli 15000/= kwa mwaka mzima.
10. Daftari ndogo moja kwaajili ya matibabu
11. Michango iliyokubaliwa na wazazi Tsh. 15,000/= meza bwaloni, Tsh. 10,000/= kuboresha taaluma
12. Mafuta ya kula lita moja.

Kwa wanafunzi wa kutwa chakula cha mchana shuleni watalazimika kulipia nusu ya gharama za chakula. Kwa wazazi watakaochagua kulipa pesa taslim walipe fedha hizo kwenye akaunti ya shule ya chakula NMB A/C Na. 70402301746 jina la akaunti ni FARM SEVENTEEN na karatasi ya kuwekea pesa (pay slip) iwasilishwe shuleni kwa Mhasibu ili apewe stakabadhi.

**VIFAA VYA MALAZI**

1. Godoro ft $2^{1}{}_{2}$ inch 4 na chandarua
2. Mashuka 2 ambayo ni sare au kulipa Tsh 18000 kwa ajili ya mashuka mawili
3. KItanda 1 ft $2^{1}{}_{2}$ au Tsh 70000/= ili achongewe kwa mafundi waliokaribu shuleni kitanda kitakuwa mali ya mwanafunzi

**VIFAA VYA CHAKULA**

1. Sahani na bakuli
2. Kijiko cha chakula
3. Kikombe cha kunywea maji

*FOMU C*

## TAARIFA KUHUSU MWANAFUNZI

(Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi na kuirejesha shuleni)

(i) Jina la mwanafunzi (aliloitumia katika mtihani wa darasa la VII. Andika kwa herufi kubwa) ……………………………………………………………………………………………………….

(ii) Kabila la mwanafunzi ……………………………… umri …………….. Jinsi ……………………..…….

(iii) Wilaya alikozaliwa mwanfunzi ………………………………….…..Mkoa ………………………..…….

(iv) Alikokulia ………………………………………..Mkoa ……………………….Tarafa ………………………

(v) Dini ya mwanafunzi ……………………………………………………………………………………………….

(vi) Tatizo la kiafya (Eleza bayana kama lipo) …………………………………………………………………

(vii) Jina kamili la Baba mzazi ……………………………………………………. Anuani ……………………..

Namba ya simu ………………………………………..kazi…………………………..umri…………………..

(viii) Jina la Mama mzazi ………………………………………………………………….Anuani ……………………..

Namba ya simu ………………………………………… kazi ………………………….umri ……………..…

(ix) Jina kamili la mlezi …………………………………………………………………. uhusiano wa mlezi na mwanafunzi ……………………………………………………………………………………………………..…

(x) Jina na anuani ya mtu anaemuhudumia mwanafunzi (mfano kumlipia michango)

Jina ………………………………………………………………………….anuani kamili ……………………………….

(xi) Baba na mama wanaishi pamoja/wametengana/yatima (KATA ISIYOHUSIKA)

(xii) Kama ni yatima, ni nani:- Wote / Baba / Mama (KATA ISIYOHUSIKA)

## AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi …………………………………………………….ambaye ni mzazi /mlezi wa ………………….…………
wa kijiji cha ………………………………………… kitongoji cha …………………………………………………

Nimesoma na kuyaelewa maagizo ya kujiunga na shule na ninakubali mwanangu asome shule ya sekondari Farm 17. Pia niko tayari kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya shule, Na nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kumsaidia mwanangu kutii sheria, taratibu na kanuni za shule wakati wote atakapokuwa anasoma shuleni.

s

Jina la mzazi/mlezi (kwa herufi kubwa) …………………………………………………………………..

S.L.P …………………………………………………………………… Simu na. ………………………………….

Saini ya mzazi / mlezi ……………………………………………. Tarehe …………………………………….

Saini ya mwanafunzi ………………………………………………. Tarehe …………………………………….

***FOMU D***

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Kila mwanafunzi anawajibika kuwa na heshima na adabu kuanzia nyumbani, mtaani, na shuleni Mwanafunzi hatakiwi kutoroka vipindi vya masomo kutumia lugha mbaya, matusi kati yake na mwanafunzi mwenzake na watu wote.

A. Kuheshimu Wimbo na Bendera ya Taifa na Nembo za Taifa kama kusimamia wima (kikakamavu) wakati wa kuimba, kupandisha na kushusha Bendera ya Taifa
B. Ni lazima kuonesha moyo wa kushirikiana, huruma, upole na kusaidiana katika shughuli mbalimbali pamoja na kazi zote za mikono.
C. Ni lazima mwanafunzi awe mwadilifu, mwaminifu na mkweli wakati wote
D. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kupokea mzigo wa mwalimu au mfanyakazi asiye mwalimu anapopita karibu yake.
E. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-
   (i) Kuvuta sigara / bangi au kutumia madawa ya kulevya
   (ii) Kuvaa mavazi na mitindo isiyo ya heshima, mfano; mlegezo, sketi fupi n.k
   (iii) Kupiga kelele darasani au mabwenini wakati wa usiku na mara baada ya kutoka kujisomea (Night preparation)
   (iv) Kunyoa mitindo isiyokubalika kama vile, fank, kipara, kiduku au kunyoa nywele ambazo haziwezi kushikika (ndogo sana)
   (v) Kufuga nywele mpaka kuwa ndefu sana, kuacha kucha ndefu na kufuga ndevu
   (vi) Utoro wa kudumu au utoro wa vipindi (utoro wa rejareja) kutofanya majaribio na mitihani, anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa
   (vii) Kuonekana anapika au kuingia jiko la shule bila sababu maalum, haruhusiwi kuingia kama si kiongozi wa zamu.
   (viii) Kuongeza mapambo au urembo nje ya sare za shule kama vile bangili, mkufu, hereni, pete, kacha (shanga za shingoni au mkononi) kujipaka rangi za kucha au mdomoni, kuweka dawa za nywele (kali) hasa wasichana
   (ix) Kuonekana katika maeneo yafuatayo; vilabu vya pombe (baa), nyumba za kulala wageni (Guest House) bila sababu maalumu, kumbi za starehe isipokuwa akiwa na mzazi/mlezi
   (x) Kumiliki au kutumia simu shuleni , kuandika maandishi ukutani au sakafuni

**F. Makosa yafuatayo yatapelekea mwanafunzi afukuzwe shule**

1. Kutumia madawa ya kulevya
2. Uasherati, kupata / kusababisha kutoa mimba
3. Wizi
4. Kushiriki vitendo vya kishirikina
5. Kukosa kwa makusudi kufanya mitihani
6. Kugomea adhabu
7. Kupiga/kupigana
8. Kudharau bendera na wimbo wa taifa, fedha za taifa na picha za viongozi
9. Utoro wa kuanzia siku (90) tisini
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya serikali
11. Kuanzisha au kushiriki mgomo

**G. AHADI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

Mimi ……………………………………………………………………….. mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga katika shule hii (Farm 17 sekondari) mwaka ……………………………………………….

1. Nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga kidato cha kwanza mwaka ……………
2. Naahidi kwamba nitatii sheria zote za shule niliyotumiwa kabla ya kujiunga na shule
3. Nitafuata masharti na maagizo yote nitakayopewa na walimu au viongozi mbalimbali wa shule

**NATOA AHADI YANGU MBELE YA MZAZI/MLEZI WANGU**

Bwana / Bibi / Ndugu ………………………………………………………………………………………………………….

Anuani yake ………………………………………………………………………………………………………………………

| | |
|---|---|
| ………………………………. | …………………………………. |
| SAHIHI YA MZAZI / MLEZI | SAHIHI YA MWANAFUNZI |
| TAREHE …………………… | TAREHE ………………….. |

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI / MLEZI…………………………………………………………**

*FOMU E*

# FARM 17 SECONDARY SCHOOL

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**FROM:**
THE HEADMASTER,
FARM 17 SECONDARY SCHOOL,
MAIL BAD 312,
**NACHINGWEA**

**TO:**
DISTRICT MEDICAL OFFICER
NACHINGWEA GOVERNMENT HOSPITAL,
P.O.BOX 30,
**NACHINGWEA.**

**OR**
ANY GOVERNMENT
RECOGNIZED HOSPITAL

**REF: MEDICAL EXAMINATION**
**(To be completed by Medical Officer)**

I have examined ……………………………………………………………………. Who aspire to join in your school as follows:-

| S/NO | AREA | REMARKS |
|---|---|---|
| 1. | Skin | |
| 2. | Eyes | |
| 3. | Ears | |
| 4. | Speech | |
| 5. | Chest | |
| 6. | Spleen | |
| 7. | Abdomen | |
| 8. | Urine | |
| 9. | Stool | |
| 10. | Hemoglobin (Hb) | |
| 11. | Inoculation against meningitis | |
| 12. | Venereal Diseases (VDRL) | |
| 13. | Neurosis | |
| 14. | Any Abnormality | |

I consider that she/he is/his not physically fit to join your school

Name and signature of Doctor …………………………………………………………

Official Stamp …………………………………………………………………………………….

Date ……………………………………………………………………………………………….